

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**WIZARA YA KILIMO**  
**TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA**

Anuani ya Simu: “Ushirika”  
Simu: +255 26 - 2322556  
Telefax: +255 26 -2321973  
B.Pepe: [ushirika@ushirika.go.tz](mailto:ushirika@ushirika.go.tz)



“Mtaa wa Kuu”  
S.L.P. 201,  
**DODOMA.**

14 Januari, 2020

*Unapojibu tafadhali taja:*  
**Kumb. Na.LA.93/288/01/59**

Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi za Vyama vya Ushirika,  
**TANZANIA BARA.**

**YAH: WARAKA WA MRAJIS NAMBA 2 WA MWAKA 2020**  
**KUHUSU MAELEKEZO YA UCHAGUZI WA VIONGOZI WA**  
**VYAMA VYA USHIRIKA KWA MWAKA 2020.**

**1.0 UTANGULIZI.**

Uchaguzi wa Wajumbe wa Bodi, Kamati za usimamizi (kwa vyama vya Akiba na Mikopo) na Wawakilishi katika Vyama vya Ushirika hufanyika kila baada ya miaka mitatu.

Kwa kuwa vyama vingi vimefanya uchaguzi wa Viongozi mwaka 2017, mwaka huu 2020 utakuwa ni mwaka wa uchaguzi kwa Vyama hivyo kulingana na mwezi ambao viongozi hao watakamilisha kipindi cha miaka mitatu cha kuwa madarakani.

Aidha inategemewa kuwa Vyama vya Ushirika ambavyo viongozi wake wanakamilisha kipindi chao cha uongozi mwaka huu 2020 wameshafanya maandalizi kwa ajili ya uchaguzi wa Viongozi hao katika Vyama husika.

Hata hivyo mwaka huu 2020 kutakuwa na uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ambapo kwa kawaida mchakato wake unaanza mwezi Julai na unahusisha wananchi ambao kwa upande mwingine wengi wao ni wanachama na viongozi katika Vyama vya Ushirika.

## **2.0 LENGO LA WARAKA.**

Waraka huu una lengo la kuweka utaratibu ambao utaepusha muingiliano katika mchakato wa maandalizi na usimamizi wa uchaguzi mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani na ule wa Viongozi wa vyama vya Ushirika, kwa kuweka kipindi maalum kwa mwaka 2020 cha kufanya uchaguzi wa viongozi wa Vyama vya Ushirika.

## **3.0 MAELEKEZO.**

Kwa Mamlaka niliyopewa chini ya kanuni ya 81 ya kanuni za Vyama vya ushirika za mwaka 2015 ninaagiza kuwa Vyama vyote vya Ushirika ambavyo Viongozi wake wanamaliza kipindi chao cha uongozi mwaka huu 2020, kufanya uchaguzi wa viongozi wa Vyama hivyo kupitia mikutano mikuu maalum kabyla ya tarehe 30/6/2020 bila kujali mwezi ambao viongozi hao wanakamilisha miaka mitatu ya kuwa madarakani. Kwa mantiki hiyo chaguzi zote za Vyama vya Ushirika ambazo zilitakiwa kufanyika kati ya Julai na Desemba 2020 zinarudishwa nyuma.

Warajis Wasaidizi wa Mkoa wanatakiwa kuhakikisha kuwa chaguzi katika Vyama vya msingi ambavyo ni wanachama wa vyama vya upili zinakamilika kabla ya kufanya kwa chaguzi hizo kwenye ngazi ya vyama vikuu na miradi ya pamoja inayohusika.

Vyama vya Ushirika ambavyo kwa mujibu wa kalenda zao chaguzi zao zitafanyika baada ya mwaka 2020 wao wataendelea na taratibu zao kama zilivyopangwa.

## **4.0 HITIMISHO.**

Waraka huu utanza kutumika rasmi kuanzia tarehe 15/01/2020.

Wahusika wote wanapaswa kuzingatia maelekezo haya na kuhakikisha kuwa Vyama vya Ushirika Nchini vinaongozwa na Viongozi waliochaguliwa kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 6 ya mwaka 2013 na kanuni zake za mwaka 2015.

Dkt. Benson O.Ndiege  
**KAIMU MRAJIS WA VYAMA VYA USHIRIKA**

**Nakala:**

Mhe: Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,  
S.L.P. 980,  
**DODOMA.**

Mhe: Waziri wa Kilimo,  
Kilimo IV Dodoma,  
S.L.P. 2182,  
**40487 DODOMA.**

Katibu Mkuu  
Wizara ya Kilimo,  
Kilimo IV Dodoma,  
S.L.P. 2182,  
**40487 DODOMA.**

Katibu Mtendaji,  
Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC),  
S.L.P. 2567,  
**DAR ES SALAAM.**

Katibu Mtendaji  
SCCULT (1992) LTD  
S.L.P 20640  
**DAR ES SALAAM.**

Mkurugenzi Mkuu,  
COASCO,  
S.L.P. 761,  
**DODOMA.**

Warajis Wasaidizi wa Vyama vya Ushirika,  
**TANZANIA BARA.**

Maafisa Ushirika wote,  
**TANZANIA BARA.**

Watendaji wakuu wa Vyama vya Upili  
**TANZANIA BARA,**